
# Ni Mtakatifu Bwana Mungu wetu

**Zaburi 137, 1-2a, 2bc-3, 4-5, 7c-8**

Musique: Innocent BISHIKWABO
Siku ya Mungu ya tano katika mwaka C




1. Nitakutukuza, ee Bwana, kwa moyo wangu wote,
   Kwani umesikia maneno ya kinywa changu.
   Mbele ya malaika nitakuimbia,
   Nitaliangukia hekalu lako takatifu.

2. Nitatukuza jina lako,
   Kwa ajili ya wema na uaminifu wako.
   Siku nilipokuita ulinisikiliza,
   Uliongeza nguvu rohoni mwangu.

3. Wafalme wote wa dunia watakutukuza, ee Bwana,
   Watakaposikia maneno ya kinywa chako.
   Wataziimbia njia za Bwana:
   Kweli, utukufu wa Bwana ni mkubwa.

4. Mkono wako wa kuume unanisalimisha,
   Bwana atatimiliza kwangu aliyonitendea.
   Ee Bwana, wema wako ndio wa milele,
   Usiache kazi ya mikono yako.